**MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MASWA**

**MKUTANO WA TAFTISHI KUHUSU OMBI LA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJISAFI ZA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MASWA: 14 FEBRUARI 2019**

## 1. UTANGULIZI

Mradi wa Maji wa Kitaifa wa Maswa ni miongoni mwa miradi 8 ya Maji ya Kitaifa iliyoko Tanzania Bara. Miradi mingine ya kitaifa ni KAHAMA SHINYANGA (KASHWASA), Handeni Trunk Main (HTM), Chalinze (Pwani), Mugango /Kiabakari (Mara), Masasi-Nachingwea, Makonde (Mtwara) na Wanging'ombe (Njombe). Mradi wa Maji Maswa unahudumia mji wa Maswa na vijiji 11 vya Zanzui, Malita, Dodoma, Mwabayanda, Mwasita, Mwabujiku, Hinduki, Buyubi, Mwadila, Iyogelo na Ng'wigwa. Eneo la mradi lina jumla ya wakazi wapatao 78,190 ambao kati yao asilimia 58 ni wakazi wa vijijini na asilimia 42 ni wakazi wa Mjini Maswa *(kwa mujibu wa Takwimu za Sensa ya Taifa ya watu na makazi iliyofanyika mwaka 2012)*. Wakazi wanaopata huduma ya maji ni 53,169 sawa na asilimia 68 ya wakazi wote. Mradi huu ujenzi wake ulikamilika mwaka 1994. Chanzo kikuu cha maji ni bwawa la New Sola lenye ujazo wa mita 4,200,000. Kituo kikuu cha kuzalisha maji kipo Zanzui na kina pampu za kusukuma maji 18, kati ya pampu hizo pampu mbili (2) zinasukuma maji kutoka Bwawani hadi kwenye chujio la zamani, pampu 16 zinasukuma maji kutoka kwenye tanki la ardhini (Clear water tank 8,000m$^3$) kwenda Maswa mjini na vijijini. Kituo kina generator mbili (2) zenye uwezo wa kuzalisha umeme (700KVA) kila moja. Pampu zote zinazotumika zimechakaa na zinafanyakazi chini ya uwezo wake halisi.

Vyanzo vingine vya maji ni bwawa la Nyanguganwa lenye uwezo wa mita 180,000 ambapo kuna pampu moja ambayo ni mpya na visima virefu vitano ambavyo vimefungwa pampu za umeme na viwili vinatumia pampu za mkono. Pampu zote za vyanzo hivi vingine ziko katika hali nzuri.

Mradi huu ulitangazwa kuwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira mwaka 1998 ikiwa ni Mamlaka ya Maji katika daraja C kupitia gazeti la serikali Na.62 la tarehe 13/02/1998. Awali Mamlaka za daraja C & B gharama zake za uendeshaji na matengenezo zilikuwa zinachangiwa na Serikali hasa kulipa mishahara ya watumishi na kulipia bili za umeme. Lakini kwa sasa Mamlaka hizi zimetakiwa kujitegemea.

## 2.0 OMBI YA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJISAFI

Gharama za huduma za majisafi zinazotumika kwa sasa zilipitishwa mwaka 2009 na tangu hapo mbali na gharama za vipuli, umeme, mabomba na viungio vyake, madawa ya kutibu maji, bidhaa za petrol kupanda mwaka hadi mwaka gharama hizi zimebaki palepale.

Kufuatia mabadiliko haya gharama zinazotumika sasa zinashindwa kukidhi gharama za uendeshaji na matengenezo pamoja na uwekezaji mdogomdogo. Aidha, Mamlaka inatakiwa kuanza kujitegemea kwenye gharama zote za uendeshaji zilizokuwa zikichangiwa na Serikali ili kuiacha Serikali kuendelea na uwekezaji katika miradi mipya.

**Jedwali Na. 1: Gharama za sasa zinazotumika**

| Kundi | Wasio na dira (Tshs/Month) | Wenye dira (Tshs/m$^3$) | GHARAMA KWA NDOO (Tshs) |
|---|---:|---:|---:|
| Majumbani | 5,600 | 445 | 9 |
| Taasisi | 9,500 | 550 | 11 |
| Biashara | 11,500 | 650 | 13 |
| Viwanda | 50,000 | 1,000 | 20 |
| Vilula (Kiosk) | 40,000 | 1000 | 20 |

**Jedwali Na. 2: Mabadiliko ya bei za baadhi ya bidhaa kati ya 2009 na 2019**

| Na. | AINA YA BIDHAA | KIPIMO | GHARAMA 2009 | GHARAMA 2019 |
|---|---|---|---:|---:|
| 1. | Gate valve ¾ “ | Pc | 6,000 | 15,000 |
| 2. | Bomba la HPDE ¾ “ Class C | m | 600 | 1,200 |
| 3. | Koki ¾ “ | pc | 7,000 | 15,000 |
| 4. | GRP Resin | Ltr | 14,000 | 19,000 |
| 5. | Calcium Hypochlorite | kg | 3,800 | 7,000 |
| 6. | Petrol | ltr | 1,600 | 2,450 |
| 7. | Diesel | ltr | 1,400 | 2,380 |
| 8. | Oils | ltr | 5,000 | 7,000 |

Ili kuiwezesha Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Maswa kumudu gharama za uzalishaji na usambazaji wa maji, matengenezo, umeme, madawa ya kutibu maji, usimamizi wa vyanzo vya maji, gharama za maabara , utawala,

mishahara ya watumishi na gharama zinginezo tumewasilisha maombi ya kurekebisha bei kama ilivyo kwenye jedwali namba 3 - 5 hapo chini.

**Jedwali Na. 3: Bei zinazoombwa kurekebishwa : 2018/2019**

| KUNDI | WASIO NA DIRA (Tshs/Mwezi) | WENYE DIRA (Tshs/$m^3$) | GHARAMA KWA NDOO (Tshs) |
|---|---|---|---|
| Majumbani | 23,960 | 1,500 | 30 |
| Taasisi | 56,750 | 2,850 | 57 |
| Biashara | 48,320 | 2,415 | 48 |
| Viwanda Vidogo | 47,100 | 1,570 | 32 |
| Viwanda Vikubwa | 314,000 | 3,140 | 63 |
| Vilula (kiosk) | 225,000 | 1,400 | 28 |

**Jedwali Na. 4: Bei zinazoombwa kurekebishwa : 2019/2020**

| KUNDI | WASIO NA DIRA (Tshs/Mwezi) | WENYE DIRA (Tshs/$m^3$) | GHARAMA KWA NDOO (Tshs) |
|---|---|---|---|
| Majumbani | 25,920 | 1,620 | 33 |
| Taasisi | 67,500 | 3,375 | 67 |
| Biashara | 52,050 | 2,585 | 52 |
| Viwanda Vidogo | 51,000 | 1,690 | 34 |
| Viwanda Vikubwa | 340,000 | 3,400 | 68 |
| Vilula (kiosk) | 253,000 | 1,400 | 28 |

**Jedwali Na. 5: Bei zinazoombwa kurekebishwa : 2020/2021**

| KUNDI | WASIO NA DIRA (Tshs/Mwezi) | WENYE DIRA (Tshs/$m^3$) | GHARAMA KWA NDOO (Tshs) |
|---|---|---|---|
| Majumbani | 30,400 | 1,900 | 38 |
| Taasisi | 74,250 | 3,720 | 74 |
| Biashara | 60,420 | 3,960 | 80 |
| Viwanda Vidogo | 59,370 | 1,980 | 40 |
| Viwanda Vikubwa | 396,000 | 3,960 | 80 |
| Vilula (kiosk) | 296,835 | 1,650 | 33 |

**Jedwali Na. 6: Ulinganifu wa bei za huduma na Mamlaka zingine za Miradi ya Kitaifa zinazotumika bila kuhusisha gharama za umeme.**

| Kundi | Mradi wa HTM (Tshs/$m^3$) | Mradi wa Chalinze (Tshs/$m^3$) |
|---|---|---|
| Majumbani | 1,360 | 1,531 |
| Biashara | 1,610 | 1,965 |
| Taasisi | 1,490 | 1,557 |
| Viwanda | - | 1,984 |
| Kiosk | - | 50Tshs/20ltrs |

Miradi hii miwili hapo juu ina mazingira ya huduma na idadi ya wateja inayoshabiiiana na Mradi wa maji wa Kitaifa Maswa.

## 3. MADHUMUNI YA KUREKEBISHA BEI

Maombi ya marekebisho ya bei yamelenga kutekeleza maagizo ya Serikali ya Mamlaka za Maji kujitegemea kwa kukidhi mambo yafuatayo:-

I. Mamlaka kuwa na uwezo wa kugharimia gharama za uendeshaji na matengenezo
II. Mamlaka kuwa na uwezo wa kutoa huduma endelevu
III. Kujenga uwezo wa uwekezaji katika upanuzi wa miundombinu
IV. Kujenga uwezo wa kutoa huduma zinazolingana na viwango vya kitaifa na kimataifa
V. Kulinda vyanzo vya maji ili viwe endelevu
VI. Kujenga uwezo wa watendaji wa Mamlaka
VII. Kuiwezesha Mamlaka kuwa na vitendea kazi vinavyoiwezesha kutoa huduma bora.
VIII. Kuongeza ufanisi wa utendaji kazi.

## 4. FAIDA ZITAKAZOTOKANA NA MAREKEBISHO YA BEI

Marekebisho ya bei za huduma ya majisafi yatakuwa na faida zifuatazo:-

I. Huduma kuwa ya uhakika na endelevu
II. Kupanua miundombinu na kuwafikia wananchi ambao bado hawajafikiwa na huduma.
III. Mauwasa kuweza kujitegemea katika gharama za Umeme na Madawa ya kutibu maji.
IV. Kumudu gharama nyinginezo za uendeshaji na matengenezo.
V. Kumudu gharama za kupunguza upotevu wa maji unaotokana na wateja wengi kutokuwa na Dira za maji .

## 5. MADHARA YATAKAYOTOKEA BEI ZISIPOREKEBISHWA

Kama marekebisho ya bei hayatafanyika kutatokea madhara yatakayopelekea huduma kufungwa kwa ajili ya mambo yafuatayo:-

I. Kushindwa kumudu gharama za uendeshaji na matengenezo na hivyo huduma kutokuwa endelevu
II. Kushindwa kutoa huduma yenye viwango vya ubora vinavyotakiwa
III. Kushindwa kufanya uwekezaji katika miundombinu

IV. Kushindwa kulinda vyanzo vya maji
V. Kushindwa kuwa na vitendea kazi bora na hivyo kazi kutokuwa na ufanisi.

## 6. HITIMISHO

Kwa niaba ya Menejimenti ya MAUWASA na Bodi ya Wakurugenzi napenda kuwasilisha hoja kwenye kikao hiki Muhimu cha kutoa maoni kufuatia ombi la kurekebisha bei za huduma ya majisafi mjini Maswa.

Imewsilishwa na,

Inj.M.T.Anaclet
Mkurugenzi Mtendaji
**Maswa WSSA**